# Uwepo wa Bwana Mungu
# (The Presence of the Lord God)

**Na**

**Terry Warford**

# Uwepo wa Bwana Mungu

## Na

## Terry Warford

## Novemba 6, 2011

# Uwepo wa Bwana Mungu

## Uwepo Wa Mungu Kihistoria

Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi kwa kula tunda lililokataliwa, walijificha kutoka kwa Mungu. Mwa. 3:8-9, "*Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu ikitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone. BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia uko wapi?*"

Mungu alimuumba mwanadamu ili awe naye. Alimuumba na kumbariki mwanadamu (Mwa. 1:28), akamweka katika bustani ya Edeni (Mwa. 2:8), akawaleta wanyama kwa Adamu ili awape majina (Mwa. 2:19-20), na akamfanyia mwanamke (Mwa. 2:21-24) tunaweza kuona kutoka katika vifungu hivi kile alichokitaka Mungu kwamba ni ukaribu na mahusiano ya kipekee na mwanadamu. Alitaka atembee nao, aongee nao, na kuwepo katika maisha yao siku hadi siku.

Lakini walipoteza bustani nzuri kwa sababu ya dhambi yao. Mwa. 3:23, "*Kwa hiyo BWANA Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa.*" Hukumu ya kifo ilipitishwa juu ya mwanadamu toka wakati ule. 1 Kor. 15:21-22, "*Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.*"

Kaini alipomuuwa Abeli, adhabu yake ilikuwwa ni kutoka katika uso wa Mungu. Mwa. 4:14, "*Tazama umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani; hata itakuwa kila anionaye ataniua.*" Ms 16, "*Kaini akatoka mbele ya uso wa BWANA, akakaa katika nchi ya Nodi, mbele ya Edeni.*"

Dhambi inamtenganisha mwanadamu na Mungu. Isa. 59:1-2, "*Tazama mkono wa BWANA haukupunguka, hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone hata hataki kusikia." Rum. 6:23, "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*"

Alafu, kupitia historia yote, Mungu aliimarisha mawasiliano na watu wake kwa njia tofauti. Heb. 1:1, "*Mungu ambaye zamani alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi.*" Aliongea

moja kwa moja na Nuhu (Mwa. 6:13-21); Alimjibu Ayubu kutoka katika upepo uliokuwa unavuma (Ayubu 38:1); Alimwita Musa kutoka katika kichaka kilichokuwa kinaungua (Kut. 3:4); Alikuwa imara, sauti ya Eliya (1 Fal 19:9-13). Na kwa njia zingine aliongea na manabii wengine, pia.

## Uwepo Wa Mungu Unaosamehe

Mat. 1:21-23, "*Naye atazaa mwana nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao. Hayo yote yamekuwa ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii ikisema, tazama bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; nao watamwita jina lake imanueli; yaani Mungu pamoja nasi.*"

Yoh. 3:16-17, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye." Hii ilifanyika kupitia kifo chake. Ms 14, "Na kama vile Musa alivyomuinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa.*"

Alikufa ili atusamehe dhambi zetu. 1 Pet. 2:24, ikiongelea Yesu, inasema, "*Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa.*"

Alitusamehe dhambi zetu ili mara nyingine tuwe na uhusiano huo wa karibu na Mungu. Kifungu kifuatacho, kinasema, 1 Pet. 2:25, "*Kwa maana mlikuwa mnapotea kama kondoo; lakini sasa mmemrudia Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu.*" 1 Pet. 3:18, "*Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa,*"

Tunapokea zawadi ya dhabihu yake kwa neema kupitia imani (Efe. 2:8-9), katika ubatizo (Efe. 2:5; Kol. 2:12). Ubatizo ndio pale kila mmoja anashiriki kifo chake, maziko na ufufuo (Rum. 6:3-6; Kol. 2:12). Hivyo dhambi zetu uoshwa (Mdo. 22:16), alafu tena sisi ni wana wa Mungu kupitia Kristo (Gal. 3:26-27).

## Uwepo Wa Mungu Unaoabudiwa

Yesu alisema katika Mat. 18:20, "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.*" Zab. 22:3, ikiongea kuhusu Mungu, inasema, "*Na wewe u Mtakatifu, uketiye juu ya sifa za Israeli.*" Ufu. 5:8, "*Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye*

*uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao anakinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.*" Kristo yuko pamoja nasi tunapomwabudu Mungu. Mungu anakaa katika sifa zetu. maombi yetu yanawakilishwa kama manukato mazuri kwa Mungu. Uwepo wa Bwana unakuwa pamoja nasi tunapomwabudu.

## Uwepo Wa Mungu Unaokaa

Baada ya kusamehewa dhambi zetu tunaweza kuwa na uwepo wa Bwana Mungu ukikaa katika maisha yetu siku hadi siku.

Mungu anakaa katika mioyo yetu. Efe. 2:22, "*Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*" 1 Yoh. 3:24, "*Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu kwa huyo Roho aliyetupa.*"

Yesu Kristo anakaa miongoni mwetu. Efe. 3:17, "*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo.*" Yesu alisema katika Yoh. 15:9-10, "*Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyoshika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.*"

Roho Mtakatifu anakaa miongoni mwetu. 1 Kor. 3:16, "*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, nay a kuwa Roho wa mungu anakaa ndani yenu?*" Rum. 8:16, "*Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu;*". Rum. 5:5, "*Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.*"

Hivyo tuna uwepo wa Mungu katika mioyo yetu kila siku, kila saa. Tunaweza kuongea naye kwa maombi wakati wowote tunaotaka. Fanya hivyo kila mara. Kol. 4:2, "*Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani;*" Na tunaweza kusikia alichokisema Mungu kwa kusoma neno lake kila wakati. 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Kifungu kinachovutia kuhusu uwepo wa Mungu unaokaa inapatikana katika 2 Kor. 13:14, "*Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote.*"

# Uwepo Wa Bwana Mungu Wa Milele

Angalia picha ya kukaa na Mungu (na Yesu) milele katika Mat. 25. Msitari wa kwanza 23, "*Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema naa mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.*" Na msitari wa 34, "*Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, njoni mlibarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu;*"

Ni mhimu hataivyo, kusoma hadithi yote ili kuona tunapaswa kuwa waamini tukifanya nini. Lakini tunachoonyesha hapa ni kwamba tukiwa waaminifu tutaishi na Mungu milele mbinguni. Yesu aliliambia kanisa la Smirna (na ahadi hii inatuhusu) katika Ufu. 2:10, "*Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi.*"

Katika. Ufu. 3:21, "*Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katika kiti change cha enzi, kama mimi nilivyo shinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*"

Katika. Ufu. 21:7, "*Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.*"

Katika. Ufu. 22:3-5, "*Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapata kuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, na watatawala hata milele na milele.*"

Kwa jina la Yesu,

Ndg. Terry Warford